




**Kuzimu na Kurudi**  
na Dr. Rawlings Documentary  
Video Transcript, [TBN Films](#)



([Mathayo7:13-14](#))

*<sup>13</sup>“Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba. Kwa maana njia inayoongoza kwenye maangamizi ni pana, na mlango wa kuingilia humo ni mpana; waendao njia hiyo ni wengi. <sup>14</sup>Lakini njia inayoongoza kwenye uhai ni nyembamba, na mlango wa kuingilia humo ni mwembamba; ni watu wachache tu wanaoweza kuigundua njia hiyo.*



**[Shahidi wa kwanza]**

Kuna watu wanaongelea kwa habari ya mwanga, kuna watu wanaongelea kuhusu kuelea juu, kuna watu wanaongelea wema na upendo, sikuhihi hayo, sikuhihia hata kimojawapo cha hayo, Nilihisi hofu kuu isiyoelezeka.

Ni rahisi kuwa atheist( mtu asiyeamini Mungu) ukiwa na mafanikio, lakini ni vigumu kuwa Atheist(mtu asiyeamini Mungu) ukiwa umelala kwenye kitanda unakaribia kufa.



**[Shahidi wa Pili]**

Nilipokuja kwa Dk. Rawlings akasema nywele zangu zilikuwa zimesimama kwa nyuma.



**[Shahidi wa tatu]**

Ilikuwa ni kitu cha kushangaza kuona kwamba kuna maisha baada ya haya maisha.



**[4th Witness]**

Kisha nikaita kwa sauti nikiwa gizani, “Yesu, niokoe!” kwa sababu nilikuwa najua labda nitakwenda Mbinguni au Kuzimu, Hakukuwa na kitu kingine zaidi hapo.



**[5th Witness]**

Sikia sauti ya mmoja aliyesikia vilio vikuu.

**[Mtangazaji]**

Kila siku watu , kama wewe na mimi, wanaishi maisha yao dakika moja na siku inayofuata wanakufa, bila ya wao kusikia au kuamini ujumbe wa wokovu. Wanasafiri kutoka dunia hii na kuingia nyingine, lakini wanachokikuta ni mateso makuu. Wanarudi na hizi ndizo simulizi zao za kweli.



[Dk. Rawlings]

Hii ni tafiti ya maisha baada ya kifo. Katika historia mwanadamu amekuwa akitabiri maisha baada ya kifo. Vitabu vyote vya dini zote vinahusu maisha baada ya kifo. Lakini wako wapi hawa? Hawa waliorudi tena kutuonyesha kwamba kuna maisha baada ya kifo?

Sasa kupitia njia za kisasa za uvumbuzi, kurejesha moyo tena, kurejesha pumzi tena, Tunaweza sasa kurejesha jumuiya yote ya watu kuongea kwetu kuna nini upande mwingine baada ya kifo. Angalia kila ambacho utafikiri

kwa habari ya mambo tunayokwenda kukuletea. Mazuri ni machache, kwa sababu watu wanapenda kusimulia mambo mazuri waliyokutana nayo baada ya kufa na kurudi.

Ushuhuda wa kuzimu ndio unaoshamgaza. Ni alama F kwenye ripoti ya matokeo, kibao cha uso kutoka kwa Mungu. Tuna baadhi ya kesi za watu watakaokusimulia wewe uzoefu wao wa Kuzimu, ili kwamba usiende njia waliyoiendea. Tunataka zaidi kukufundisha jinsi ya kuanza upya katika moyo wako; kuanzisha upya pumzi ya mtu aliyekufa mara. Zingatia kwamba kifo kinaweza kurudishwa; Una muda wa dakika 4 za muhimu kabla ya seli za ubongo hazijaanza kufa kwa sababu ya kukosa mzunguko wa damu, na kabla ya kukakamaa hakujaingia.

Nimeona vifo viwili, ambavyo vilihitaji ufufuo, kitu ambacho mwanadamu hawezi kufanya. Tunaweza kufanya tu urekebishaji (resuscitation) kitu Mungu alichoruhusu tukifanye. Ni uzoefu gani wa kuzimu uliokuwa unahusu mazungumzo ya mtu na wokovu wakati wakiwa chini, na mtu akakumbuka mazuri tu? Hii haikuwa kesi kwa Ronald Reagan. *(Haihusiani na raisi mstaafu Ronald Reagan)* Alikuwa na mtoto wake wa kiume mdogo, alipokuwa akienda kwenye stoo ya 7-11, akaingia kwenye mzozo, na kulikuwa na chupa iliyokuwa imevunjika, na akawa nameraruliwa kwa chupa na huyo mvamizi wake.



*===Ronald Reagan ===*

### [Ronald Reagan]

Mwaka 1972 mke wangu alivunjika moyo. Nilikuwa ni mtu wa madawa ya kulevya. nilikuwa ni mtu wa jela. Familia yangu ilivunjika moyo. Mke wangu alijaza hati ya talaka mara nyingi. Watoto wangu waliniogopa. Sikuweza kukaa na kazi, hali ya kichwa change iikuwa mbovu sana. Nilikuwa katika hali hii ya maisha nikamchukua mtoto wangu wa miaka 6 tukaenda soko dogo kununua vitu. Tulipokuwa njiani, nikamuona kijana, anatoka nje ya mlango. Mara mzozo ukaibuka na baada ya muda tayari nilikuwa nimempiga kwenye kichwa. Akawa ameanguka kwenye mkusanyiko wa chupa. baadhi ya chupa zikapasuka na haraka akachukua chupa akaanza kunirarua nayo. Nikanyanyua mkono wangu wa kushoto ili nijaribu kuzuia mrusho wa ile chupa lakini hata hivyo chupa ile ilinikata vibaya kwenye nyama za mkono na mishipa mikubwa ya mkono. Nilianza kuvuja damu mithili ya kufa kwa muda mchache tu. Lakini nikiwa bado na hasira, chuki na gadhabu, nikaendelea kupigana na ikaendelea kutoka. Mtoto wangu mdogo akaanza kupiga mayowe, alikuwa kama amepagawa.

Mmiliki wa stoo ya 7-11 akaja na kunieleza kuwa kama sitakwenda hospitali mapema, nitavuda damu na kufa muda mchache tu. Hivyo akanichukua kwenye gari yangu na tukaondoka. Tulipokuwa kwenye chumba cha tahadhari (emergency room) nilikuwa sijitambui vya kutosha. Madakitari walipoanza kunishughulikia, nilikuwa nasikia sauti zao, walikuwa wanasema “*hatuwezi kumsaidia, anatakiwa apelekwe hospitali nyingine. Inawezekana tutapoteza mkono wake.*” Muda tu waliponiingiza kwenye gari ya wagonjwa (ambulance), Mke wangu alikwisha fika na tukaenda pamoja kwenye ambulance.

Lakini walipokuwa wakivuta kutokea kwenye maegesho ya hospitali, Muuguzi kijana akaangalia sura yangu, na nilimuona kwa mbali kwa kuwa nilikuwa dhaifu tayari. Akasema “*mkuu, unamwitaji Yesu kristo*” Sikuwa namjua Yesu Kristo. Sikuwa nafahamu kitu gani alikuwa akiongea, kwa hiyo mimi nikaanza kulaani. Mara tena akaniambia “*Unamuhitaji Yesu!*” Alipokuwa akiongea nami, ilionekana waziwazi kama Ambulance imewaka moto. Nilifikiri kabisa imekwisha waka. ilijawa na moshi na haraka nilianza kushuka kwenye moshi, kama kwenye tanuru. Baada ya muda, kutoka katika moshi na kutoka kwenye giza nilianza kusikia sauti za watu. Walikuwa wakilia, wakipiga mayowe, wakigugumia. Nilipokuwa nikiangalia chini, ilikuwa kama shimo la volikano. Niliona moto, moshi na watu ndani ya hili shimo la kuungua. Walikuwa wakipiga mayowe, wakigugumia, na kulia. na walikuwa wakiungua kama hawaungui yaani hawaishi. Nikaanza kwenda chini kwenye hili shimo.



#### [Wife, Elaine Reagan]

Alikuwa akipigana, akipigania kitu kama kuomboleza na kugugumia. kulikuwa kama kuna vita inaendelea. Sikuwa Mkristo kwa wakati huo. na sikufahamu chochote kwa habari ya vita vya kiroho. ilikuwa inatisha kwangu mimi kwa sababu nilikuwa ninaihisi. Ilikuwa kama mwanga na giza. Alikuwa kama anapigana na kitu fulani. Sikujua ilikuwa ni nini, lakini sasa najua, alikuwa akiona maono ya kuzimu.

#### [Ronald Reagan]

Lakini kitu cha kushangaza ni kuwa nilianza kutambua watu wengi, waliokuwa kwenye miali hii ya moto. Ilikuwa kama lenzi ya kamera ikinionyesha sura zao, zilikuwa karibu. Niliweza kuona miili yao, niliona wanavyoomboleza, maumivu na mataabiko. Wengi wao wakaanza kuita jina langu, na kusema “*Ronny, usije mahali hapa, hakuna namna ya kutoka. Hakuna kutoka tena kama ukija mahali hapa*”.

Niliangalia katika sura ya mtu mmoja aliyekufa kwenye wizi, alipigwa risasi na kuvuja damu mpaka kufa pembeni mwa barabara, niliangalia sura ya vijana wawili ambao walikufa kwa ajali ya gari wakiwa wamelewa. Niliangalia sura za wengine ambao walikufa kwa kuzidisha madawa ya kulevyia, ambao mara ya kwanza nilikuwa na ushirika nao. Walikuwa wakionyesha wanalia na maumivu, lakini nilichoamini zaidi ilikuwa ni upweke mkuu. Upweke ulikuwa ni mkubwa sana, kiasi kwamba hakukuwa na matumaini yeyote, hakuna kutoka, hakuna jinsi ya kutoka katika eneo hili. Harufu ilikuwa kama ya sulfur, kama umeme wa kuchomelea, harufu ilikuwa mbaya sana.

Katika maisha yangu, nimeona watu wakiuawa, nimekwishashirikishwa katika mapambano ambayo watu waliuawa. Nimekuwa gerezani kwa kesi ya kuua. Nimekulia katika shule ya marekebicho, na katika jela. Nimewahi kupigwa bila huruma na baba aliyekuwa na hasira na matatizo ya pombe wakati nikiwa mtoto. Nilitoroka nyumbani nikiwa na miaka 12 na nilikuwa najisikia kuwa hakuna cha kunibabaisha katika dunia hii. Maisha yangu yalikuwa yameshindikana, ndoa yangu ilikuwa imeshindikana, afya yangu ilishindikana. lakini sasa nilikuwa naona kitu ambacho kiliniogopesha mithili ya kufa, kwa sababu sikuelewa. na nilipokuwa nikiangalia katika shimo hili, hii sehemu ya moto, makelele, vilio na mateso, niliishiwa nguvu katika giza.

Nilipo fungua macho, nilikuwa niko hospitalini katika chumba pale Knoxville; Tennessee na mke wangu amekaa pembeni. Kulikuwa na mishomo ya nyuzi kwenye mwili wangu, mkono wangu ulikuwa umetengenezwa. nilikuwa na nyuzi karibu 100. Niliangalia uso wa mke wangu. Nilikuwa nafikiri mahali nilipo, au kitu chochote kilichokuwa karibu yangu. Nilipokuwa nikiwaza ilikuwa ni kuhusu kile nilichokiona.

#### [Elaine Reagan]

Alikuwa na uso wa kushangaa, na ulikuwa ni unaogopesha. Na akasema, “*Sifahamu kitu gani kimenitokea, lakini nimekuwa kwenye sehemu ya kutisha.*” Na nikazidi kumueleza “*Ulikuwepo hapa hospitali, umekuwepo hapa hospital wakati wote huu*” Na akazidi kusema, “*Hapana, nimekuwepo kwenye sehemu nyingine. Sifahamu ilikuwa ni nini, lakini ni ya kutisha, sehemu ya kutisha,*”

### [Ronald Reagan]

Nilikuwa bado nasikia makelele(vilio). Nilikuwa bado nasikia harufu mbaya. Nilikuwa bado nahisi moto, Nilikuwa bado nasikia sauti za watu niliowajua wakiniililia nirudi. Siku zilizofuata, nilijaribu kuondoa hilo ndani ya fikra zangu. Nilijaribu kuwa mlevi, lakini sikuweza kulewa, nilijaribu kutumia madini, lakini sikuweza kulewa, Nilijaribu kila kitu ili kuondoa kicho kitu ndani ya fikra zangu na sikuweza.



Asubuhi, miezi michache iliyofuata, nilikuja nyumbani mahali ambapo mke wangu alikuwepo. Nilijaribu kuwa mlevi, lakini sikuweza kulewa. Nilipokuwa natembea ndani ya nyumba na kurudi chumbani, taa ilikuwa imewashwa. Mke wangu alikuwa amekaa chumbani, na alikuwa na kitabu kikubwa kimefunguliwa kwenye mapaja yake. Alinitazama na uso wake ulikuwa unang'aa. Na akasema, *“Ronny, usiku huu Nimempokea Bwana Yesu Kristo kama mwokozi,”*

Haikumpasa kusema maneno mengi sana kwangu, maisha yetu yalikuwa yamejawa na maumivu. Yeye alikulua Chikago; Baba yake alikuwa ni Mhudumu wa bar kusini mwa Chikago. Hakuwa anafahamu chochote kuhusu Mungu, au kanisa au dini. Maumivu yalijionyesha kwenye sura yake, kwenye mikunjo ya uso kwamba nilikuwa nikimfanyia ukatili, vurugu, ulevi na madawa ya kulevywa. Wakati mwingine nilikuwa nikiondoka kwa muda wa miezi, yeye pamoja na watoto walikuwa hawana wazo ni wapi nilikuwa. Lakini sasa uso wake ulibadilika. Mikunjo ya uso ilikuwa kama imeondoka kabisa, tabasaamu lilichukua nafasi ya majonzi na maumivu. Alinitazama na kuniambia, *“Yesu ameniokoa usiku huu. Je ungependa kwenda nami na kusikia kwa habari ya huyu Yesu.”* nilijiwazia mwenyewe, *“Nimejaribu kila kitu kwenye maisha haya, hakuna kilichofanya kazi kwangu mimi. Watu ninaowapenda zaidi, mke wangu, watoto wangu, ni mkorofi kwao.”* kwa hivyo nilikubaliana nae.



Wiki chache baadae sku ya jumapili asubuhi, Novemba 2, 1972, kabla ya saa sita asubuhi, mhubiri akasimama na akasoma katika biblia. Nilikuwa nimekaa nyuma ya jengo, Sikuwa najua chochote nje ya biblia, na akasoma katika Kitanu cha Yohana. akaanza kusoma maneno haya *“Tazama mwanakondoo wa mungu achukuaye dhambi ya ulimwengu”* aliposema hivyo *“mwanakondoo”* akanifanya nimsikilize. Ujumbe mwingine wowote usingekuwa na maana kwangu, lakini aliposema *“mwanakondoo”* aliupata na huu moyo mgumu wa huyu mwenye dhambi.

Nilipokuwa nina miaka 9, mtoto maskini sana katika milima ya mashariki ya Tennessee, na baba ambaye alijua hasira tu, ukatili na pombe, jirani yetu alinipa kondoo mdogo. na nilikuwa nikitembea maili mbili ili kuwahi basi la shule. Siku moja nilipokuwa natembea kutoka kwenye yadi yake alinisimamisha na akasema, *“mwanangu nina zawadi kwa ajili yako”* na akanionyesha huyu kondoo mtoto.

Nilimchukua huyo kondoo mpaka nyumbani. Alikuwani rafiki yangu, Rafiki pekee niliyekuwa naona ninae. Alikuwa ni rafiki kweli, katika siku zilizofuata mbele alikuwa akinifuata, alikuwa akinipokea nilipokuwa nashuka kutoka katika basi la shule. Kondoo huyu alitembea kwenye vichaka na mbao kuja kunipokea.



Siku moja jioni nilipokuwa narudi nyumbani, kondoo hakunipokea. Nilimsikia baba yangu akilaani na kupiga kelele, alikuwa akifanya kazi kwenye gari ambayo ni model ya zamani, alikuwa akibadili tairi kwa mikono yake. Nilipokuwa nikitembea kumfuata kwa sababu sikutaka kutukanwa. nilijaribu kumpita, lakini nilipokatiza upande mwingine wa gari, nilitazama chini na

tazama alikuwa ni kondoo wangu ametapakaa damu mwilini kwenye ngozi yake nyeupe. kulikuwa na alama ya tairi iliyokuwa imepita juu yake. Kondoo alikuwa amekuja kwenye gari akiwa na shauku ya kuona , na katika hasira ya pombe zake, baba yangu alipitisha tairi lake la chuma juu ya kondoo.

Nilipoona kondoo wangu, rafiki yangu, amekufa, nilianza kupiga mayowe, nilikimbia kwenye msitu nikilia kwa mayowe. *“ameua kondoo wangu, ameua kondoo wangu!”*



Katika umri wa miaka 9, chuki na vurugu vilichukua maisha yangu, vikanimiliki. kutokea siku hiyo, sikuwa tena mtu wa kawaida. Katika umri wa miaka 12 nilikuwa mkimbizi. Nilikuwa katika mfumo wa juvenile, nilifungwa mara kwa mara. Sikuwa na heshima na mamlaka. Nilimchukia kila mtu aliyekuwa akionyesha mamlaka juu yangu. Lakini nilipokuwa na miaka 15, nilikuwa jela kwa wizi wa gari, kwa kuiba. Katika umri wa miaka 15 nilifungwa kwa kesi ya mauaji; baada ya kuhusika katika ajali ya gari ambayo iliua baadhi na kuwaacha wengine wamekuwa walemavu. Wakati huo nilishangaa sijui kama maisha yanaweza kubeba chochote cha muhimu kwangu.

Sasa muhubiri akataja *“Mwanakondoo”* aliupata usikivu wangu. Akasema Yesu ni Mwana kondoo wa Mungu, alikufa na kumwaga damu yake ili kwamba yeyote atakaye, anaweza kuwa na mwanzo mpya. Kutakuwa na msamaha na kuanza upya.




Asubuhi hiyo, nilipokuwa nimesimama na kujaribu kuondoka nje ya jengo la kanisa, niliwaza, *“ Sitaki kuona mtu akiniangalia ninalia. Sijawahi kulia tokea kipindi kile nina miaka 9. Siogopi chochote kinachoishi kwenye dunia hii, na hivyo sitaki kumuona yeyote akiniona ninalia.”*

Nikageuka ili niondoke, lakini tena nikasimama kwenye mlango wa kutokea mbele ya jingo. Sikuwa nafahamu sala ya toba ya mwenye dhambi. Sikuwa nafahamu njia ya warumi ya wokovu. lakini sala yangu ilikuwa ni hii, *“ Mungu kweli kama unaishi, tafadhali, niue au niponye. Sitaki kuishi tena, mimi sio mume, mimi sio baba, sina uzuri wowote.”* Na kuanzia wakati huo, ilikuwa kama giza na weusi umeondoka katika maisha yangu. Kisha machozi yalianza kutoka na kwa mara ya kwanza tokea nikiwa na miaka 9, machozi yalimiminika. Hukumu ya dhambi ikaondoka moyoni mwangu, vurugu, hasira na chuki vikaondoka kwenye maisha yangu. na Yesu Kristo akawa Bwana na mwkozi wa maisha yangu asubuhi ile. Baada ya asubuhi njema nilipokuwa nimempa maisha yangu Yesu Kristo, Sikufahamu kitu ambacho kingetokea. Mungu aliponya fikra zangu, ufahamu wangu, athari ya madawa ya kulevyaa; Ulevi uliondoka mara, nilikombolewa. Na kutokea siku hiyo nikajua imenipasa kusimulia historia ya kile kilichonikuta. Maisha yangu yaliachwa ili kuwaeleza wengine kwa habari ya sehemu hii niliyoiona, na tumaini kwa Yesu Kristo kuokoa wanadamu kutoka katika uharibifu huu mbaya.

---

=== OBE & NDE ===



### [Dr. Rawlings]

Hapa tena tunashangaa kuzimu ni kwa watu wabaya au watu wazuri. Nitapenda nitambulisha somo la OBE (out of body experience). na NDE (Near Death Experience). Unafahamu nini kifo cha kliniki kinavyofanana, Pale moyo uaposimama, pumzi inasimama, lakini pia tunaanza maisha tena. Unaanzisha pumzi tena na Moyo, a mtu anakuja tena kutoka kwenye kifo. Hali ya kurudi kabla ya kukakamaa (rigor mortis) akujiaingia

Lakini OBE( uzoefu wa nje ya mwili) na NDE( Uzoefu wa karibu na kufa) uko tofauti sana. Near Death Experience (NDE) ni kama nikishika bunduki na kusema “*nipe fedha zako*” unaweza ukaogopa kiasi cha kufa, lakini hauendi popote baada ya kufa. Mara nyingi gari zinapotaka kugongana, ni uzoefu wa karibu na kufa, lakini hakuna kinachohusika kusimamisha mapigo ya moyo, au kusimamisha pumzi. Na bado, waandishi wengi wanaoandika vitabu kuhusu vipengele hivi vya OBE na NDE wanavijumuisha bila ya kifo cha hospitali/kliniki. Tunajaribu kuchunguza kifo cha kliniki, ambapo watu hufa kabisa na wanakuja tena kwenye maisha.

Sasa uzoefu wan je ya mwili ni njia ya kwenda kule bila ya kufa. Jinsi gani ungependa kufahamu jinsi kifo kinavyokuwa ,bila ya kufa?

- kwa kufanya Deep hypnosis unaweza ukajua.
- kwa kupata uzoefu kutoka kwa walimu wa kiroho (guru) wa India, ukajifunza mbinu za kufanya meditation pamoja na nyombo( mantra).
- Unaweza ukapata chemical hypnosis.
- unaweza ukafanya Skrying na mpira wa crystal.
- Unaweza ukajaribu msisimuko wa umeme.
- *[Tafadhali usijihusishe na yoyote kati ya haya.]*

Kuna njia nyingi za kutoka nje ya mwili, kushuhudia maisha nje ya mwili, kujitenga roho na mwili. Hii ni maana kutoka kwenye biblia, pale roho inapojitenga na mwili. Lakini tunaongelea kwahabari ya kujitenga moja kwa moja, na sio mtu mwenyewe anajitenga, Na sasa hatuongelei kuhusu NDEs na OBEs ,tunaongelea **kifo cha kliniki**. Hii ndiyo ambayo watu wengi wamepitia.

---

### === Charles McKaig ===


Moja kati ya kesi hizi ni Charles McKaig, miaka 57 mbeba barua. Alipatwa na maumivu ya kifua. Tukampeleka ofisini: tukamweka kwenye Tread mill, mpaka pale alipopatwa na maumivu ya kifua tena. Alijishikamanisha na EKG (Electrocardiogram/heart monitor), EKG ikaenda vibaya/ikaharibika. Tunafahamu alipatwa na maumivu ya kifua, lakini kabla hatujasimamisha mashine, akadondoka akafa.

Lakini alipodondoka akafa, alikuwa na hali ya tofauti sana. Alitetemeka kama watu wengine wanavyokuwa wakifanya wanapokuwa wakifa na moyo unapokuwa ukisimama kupeleka damu kwenye ubongo. Macho yake yalizunguka, Akawa wa bluu, akaacha kupumua. Nesi akaanza kumfanyia IV nami nikaanza kumfanyia masaji ya moyo wan je. Kitu cha kushangaza kikatokea, nilipoacha tu kumfanyia (resuscitate) na kumweka kwenye pace maker.



### [Charles McKaig]

Nilipokuja kwa Dr. Rawlings alisema nywele zangu zilikuwa zimesimama kwa mwisho, macho yangu yalikuwa yameanza kuwa makubwa.



Nilikuwa naogopa sana kiasi cha kufa. Nilishtuka sana.

Maisha yangu yalikuwa kawaida tu, nilijirusha sana tu. Nilikuwa ninashiriki kanisani wakati niko mdogo, kwa sababu ya wazazi wangu. Sikuwa nimefahamu kanisa lilihusu nini hasa, au kumpokea Kristo ilikuwa ni nini hasa.

Asubuhi moja nikiwa kazini nilitembea mpaka kwenye kliniki moja pale mtaani kwangu. Kwa wakati huo nilifikiri kuwa ninaweza kuwa na mapigo ya moyo. Hivyo nilikutana na Dr. Rawlings. Aliniweka pale kwa muda wa kama siku 3 mpaka 4. Na aliponifanyia kipimo cha msongo wa mawazo (stress test). Naakumbuka nilipokuwa nikifanyiwa kipimo hicho nilikuwa naona kama nitoke katika kipimo hicho, na hicho ndicho kitu cha mwisho nakikumbuka nilijisikia.



Nilipokuja kwa Dr. Rawlings alikuwa akinipa CPR, na akaniuliza tatizo ni nini, kwa sababu nilikuwa naonekana naogopa sana. Nilimweleza kuwa nilikuwa kuzimu na nina hitaji msaada! akanieleza kwangu mimi, “*Kaa na kuzimu yako, mimi ni dakitari na ninajaribu kookoa maisha yako, unahitaji muhubiri kwa ajili ya hilo*” Alipokuwa akinipa CPR, alikuwa akijaribu kuunganisha pacemaker kwa mkono mwingine. Niliishiwa nguvu ya kutoweka kwa mara moja, kisha nitakazia CPR na kurudi tena.

Mara nilikuwa nikielea hewani, nikiangalia nini kilichokuwa kikiendelea, nikiangalia chini. Kila nikirudia mwili wangu nilikuwa nikisema, “Tafadhali mnisaidie, tafadhali mnisaidie, sitaki kwenda tena kuzimu.” Kisha nesi aliyekuwa anaitwa Pam akasema, “*Anahitaji msaada, fanya kitu!*” Wakati huo Dr. Rawlings aliniambia nirudie haya sla ile fupi. “*Ninaamini Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Yesu, okoa nafsi yangu. Nifanye niwe hai. Kama nikifa tafadhali nitenge mbali na kuzimu!*”

Baada ya hili, Upande mwingine katika uzoefu wangu huu wa kukaribia kufa ulikuwa mzuri sana. Nilimwona mama yangu wa kambo, mama yangu. Mama yangu alikufa nilipokuwa na umri miezi 5. sikuwahi kuona picha yake. Mama yangu wa kambo amekufa miaka 10 iliyopita. Sikuwa tunawasiliana lakini walikuwa wakinyoosha mikono yao ili inifikie.

Nimesikia wakisema haukuweza kuja na fedha, Nilipokuwa na mama na mama yangu wa kambo, niliona hawakuwa na mifuko. Nadhani hii inaonekana si kitu cha kawaida lakini natajihidi kukumbuka kila kitu nilichokiona.

Baada ya hapo, nakumbuka nilitembea kuelekea chini kwenye njia ambayo ilikuwa ina rangi pande zote, rangi nzuri sana zinazong’aa. Kulikuwa na mwanga mmoja ambao ulinizugukana kunilinda. Sijawahi kujisikia vizuri na salama kwenye maisha yangu kama nilipo kuwa pale.

### [Dr. Rawlings]

Baada ya haya kuisha, nilijua kilichotokea. Kulikuwa na mabadiliko mawili. Sio tu kumfanya huyu atheist (asiyeamini Mungu) aliyekuwa chini ya sakafu akipata matibabu lakini pia ilimfanya huyu dakitari atheist aliyekuwa akishughulika naye. *(Dr. Rawlings anajiongelea yeye mwenyewe)*. Hii ndiyo sababu pekee iliyonifanya nitokeze mbele zenu sasa, kuwaeleza kwamba kuna maisha baada ya kifo. Na sio yote ni mazuri.



Wengi wenu mnaweza mkasimulia tofauti kati ya kuondoka kwa muda, kifo cha kliniki na kifo cha kibaiolojia. Chukulia kesi ya Charles McKaig. Alikuwa kwenye mashine ya kukimbia na ninaweza kukueleza kuwa alikuwa kwenye kifo cha kliniki. Alikuwa na swali lililokuwa kwenye uso wake, alikuwa yupo karibu kuuliza swali hilo. Lakini



nilimtazama tu kimzaa. Alipokuwa akitembea kwenye mashine niligundua kwamba moyo wake ulikuwa umesimama. na pumzi yake pia ilisimama. Alikuwa akiendelea kutembea na kuongea kwa dakika moja au mbili hivi kabla ya kukosa damu kwenye ubongo kulipomfanya adonoke na kufa. Alikuwa amekufa lakini hakuwa anafahamu. Nilitakiwa kuwa nimemueleza.

Baada ya muda mfupi tulianza matibabu ya kliniki ya mtu anaye kufa(CPR). Tuliuanzisha moyo kwa mara nyingine tena na akarudi tena. Hii ilikuwa hakika ni kifo cha kliniki. Sasa kifo cha kibaiolojia kingetokea baada ya muda wa dakika 4-6 hazijapita baada ya kifo cha kliniki. Kwa sababu ya kukosa oksijeni kwenye ubongo, seli za ubongo zinakufa; Ni seli zenye nguvu sana katika mwili. kasha baada ya hapo rigor motis inakuja na mtu anakuwa amekakamaa kama ubao. Na sasa tunakuwa tunahitaji ufufuo kwenye hali hiyo, ni Mungu pekee anayeweza kufanya ufufuo, Ni Mungu pekee anayeweza kufanya ufufuo, Sisi tunaweza tu kufanya resuscitation (uhamsho). Kitu ambacho tumepewa kuweza kufanya.

---


### === Howard Storm ===

Howard Storm alikuwa ni profesa aliyekuwa Paris na darasa lake, alipokuwa amepatwa na matatizo yaliyosababisha mpasuko wa tumbo, mpasuko wa maumivu, peritonitis, shock, kifo cha ghafla, kifo cha hospitali, resuscitation, na uzoefu wa kuzimu.



[Howard Storm]

Nilikuwa na miaka 38 nikiwa kama professor wa chuo, nikifundisha mchepuo wa art. Niliwachukua wanafunzi wangu na mke wangu mpaka Ulaya. Tulikuwa tumefanya safari ya wiki 3, na hii ilikuwa ni siku moja kabla ya mwisho. Tulipokwa Paris, mida ya saa 11:00 asubuhi, nilipatwa na tatizo kwenye tumbo langu. Ilikuwa ni maumivu makali sana ambayo sikuwahi kuyapata katika maisha yangu, kiasi kwamba yaliniangusha chini.



Hivyo nilikuwa nikijivingirisha, nikilia kwa sauti, nikiomboleza, na kujipiga na kukoroma pale sakafuni, mke wangu akaita huduma ya wagonjwa (emergence).

Dakitari akaja na akachukua gari ya wagonjwa (ambulance) kwa sababu alijua ilikuwa ni tatizo gani. Gari ikanichukua maili 8 kutoka pale tulipokuwa mpaka hospitali ya umma. Kisha nikachukuliwa katika chumba cha huduma ya haraka na kuchunguzwa na nikachunguzwa na madakitari wawili zaidi, waliojuwa kabisa tatizo lilikuwa ni nini. Kisha nikaenda kwenye upasuaji. Kwa sababu hakukuwa na mpasuaji, Niliwekwa pale nimsubiri. Kwa hivyo nilikaa pale kwa muda wa masaa 8 mpaka 10 nikiwa hospitali bila ya matibabu, uchunguzi, hakuna huduma, nikisubiri mpasuaji aje na kunifanyia operesheni kubwa.

Sasa ilikuwa ni saa 8:30 usiku na nesi akaja na kuniambia kwamba wanasikitika hawakupata dakitari kwa ajili yangu na kwamba wangenipatia siku inayofuata. aliposema hivyo, Nilijua kuwa sasa ndio nimefikia mwisho wangu, nilijua nimekufa tayari. Kitu kilichonifanya niwe mzima ni kwamba sikutaka kufa. Unajua nilikuwa ni atheist (mtu asiyeamini kama kuna Mungu), sikuwa naamini, mtu anayeishi kwa mafanikio yake mwenyewe.

Mbali na maumivu, kufa ilikuwa ni kitu kibaya ambacho kingenitokea kwa sababu ilikuwa ni mwisho wa maisha, na hakukuwa na kitu chochote zaidi. Lakini aliponiambia kuwa mpasuaji angekuwepo mpaka siku iliyofuata, wazo likanijia la kuishi dakika na saa nyingine kwa maumivu yale ilikuwa si kitu kwangu tena. Nilining'inia kwenye tumaini la kuwa watanipatia dakitari na kunifanyia upasuaji, anifungue na kuondoa

tatizo. Lakini waliposema hawakumpata dakitari, nikamueleza mke wangu kwamba ilikuwa ni wakati wa mimi kusema kwa heri kwa sababu nilikwenda kufa.

Kwa hiyo akaamka na kuniwekea mikono yangu , na kuniambia jinsi anavyonipenda na nikamueleza jinsi ninavyompenda, ilikuwa ni wakati wa huzuni sana. Tukaagana kwa heri. Tuliongea vile vitu ambavyo vilitokea kwa muda wa miaka 20 ya pamoja.



Kisha akakaa chini kwa sababu alijua sasa ilikuwa ni mwisho nami nilijua hivyo pia. Ilikuwa ni vigumu kumuangalia akilia vile, nikafunga macho yangu ili niondoke. Nikawa sijitambui. Nilikuwa sijitambui kwa muda kitambo tu, muda mchache bila shaka.

Kisha nikawa najitambua tena. Nilifungua macho yangu na kuangalia n ilikuwa nimesimama pembeni mwa kitanda change. Nilifahamu kabisa nilikuwa wapi, na hali gani nilikuwa nayo, hakukuwa na mchanganyo wowote katika akili yangu. Nilijisikia mzima kabisa, Mzima zaidi ya jinsi nilivyoweza kujisikia kwenye maisha yangu. Watu waliniuliza, “*ulikuwa ni mzimu*” Niliwaeleza tofauti, nilikuwa nikijitambua kabisa.

Nilipokuwa nikiangalia mle chumbani, Niligundua kuwa kuna kitu chini chini ya shuka pale kitandani, mwili. Nikainama ili kwenye kitanda ili niangalie sura , nikaona kuwa ianfanana nami. Lakini haiwezekani, mimi mbona ni mzima, niko na nguvu na ninajisikia vizuri tu. Nilijaribu kumueleza mke wangu, lakini hakunisikia wala kuniona mimi. Nikafikiri kwamba alikuwa akinipuuza. Hivyo nilikuwa na hasira naye , kwa kunipuuza.

Kwa hiyo nikaanza kupiga makelele na kumkoromea, “*Kwa nini kuna huu mwili kwenye kitanda ambao unafanana na mimi?*” Umefikajefikaje mahali pale? Nilipatwa na hisia ngumu kwamba mwili ule ulikuwa ni mimi, lakini ilikuwa inaogopesha kufikiri hivyo. Kwa hiyo nikaanza kuhaha kwa sababu hii yote ilikuwa si kitu cha kawaida. Haiwezekani ikatokea hii, haiwezekani; nilikuwa na gauni la hospitali nimevaa, na kila kitu kilikuwa halisi.

Nilisikia watu wakiniita kwa nje ya chumba, wakiongea katika sauti laini. “*Howard, imekupasa kuondoka pamoja nasi sasa. Njoo haraka, njoo hapa nje,*” Hivyo nikaenda kwenye njia ya mlango wa chumba. Kulikuwa na watu nje ya njia ya jengo. Njia ilikuwa ina ubaridi, ni ya kijivu, si ya mwanga au giza, ni ya kijivu. Watu wote hawa wanaume kwa wanawake walivaa nguo za kijivu. Unaweza ukadhani ni sare za hospitali. Niliwauliza kama walikuwa ni kutoka kwa madaktari ili wanipeleke kwenye chumba cha operesheni. Niliwaeleza kila kitu kuhusu hali yangu na jinsi nilivyokuwa nikisubiri. Waliendelea kusema, “*Tunafahamu, tunafahamu. Howard njoo upesi, njoo pamoja nasi, tumekuwa tukikusubiri*”.

Niliondoka kwenye chumba ambacho kilikuwa kinaangaza na mwanga mkali, na nikaenda katika barabara ya ukumbi ambayo ilikuwa baridi na isiyoangaza. Niliwafuata watu hawa; ilikuwa safari ndefu sana. Hakukuwa na wakati, na wakati narejea muda, nilidhania tu kwa sababu kulikuwa hakuna wakati katika eneo hili. Lakini sehemu hii, kama ilikuwa ni kufanya mazoezi , ingekuwa sawa na kutembea kutoka



Nashville mpaka Louisville (175 miles, 281 km) kutembea na watu hawa.



Tulipokuwa tukitembea walikaa karibu yangu, niliendelea kusonga mbele, na iliendelea kuwa giza na giza. Walianza kuwa maadui waziwazi zaidi na zaidi kwangu. Mara ya kwanza walikuwa wazuri na watamu ili kunipata niende pamoja nao. Kisha nilipokuwa naenda nao walisema vitu kama, “*haraka, endelea kusonga, fungua mdomo, acha kuuliza uliza maswali*” hali iliendelea kuwa mbaya.

Hivyo tuliingia katika giza tororo nami nikahofu kabisa. Watu hawa ni maadui sana na mimi sijui niko wapi. Nikasema, "*Sitakwenda na nyie zaidi ya hapa.*" Walisema, "*tumekaribia na hapa.*" Tukaanza kupambana nikijaribu kutoka mbali nao. Walikuwa wakisukuma na kunivuta. Sasa walikuwa wengi. Mwanzo walikuwa watano, sasa pamoja na giza inaweza kuwa 100s au 1000s, sikujua.



Walikuwa wakicheza na mimi. Wangeweza kuniharibu



kama wangetaka, lakini hawak utaka. Walitaka kuniwekea ma umivu ndani yangu, kwa sababu wao wanaridhika kwa maumivu niliyoyapata. Ni vigumu sana kuongelea na sitawaambia kuhusu uzoefu huo, ilizidi kuwa

mbaya. Awali walikuwa wakinarua kwa kucha zao, walinikwarua, ng'ata na kuuma. Nilijaribu kujitetea mwenyewe, nilijaribu kupambana nao na niondoke katikati yao lakini ilikuwa ni kama niko katika mizinga ya nyuki, walikuwa mamia juu yangu. Mara nilikuwa nimelala kwenye uwanja; nikiwa nimeraruliwa kila sehemu ina maumivu, ndani na nje. Ilikuwa ni vigumu sana kuvumilia maumivu ya mwili lakini ilikuwa ni maumivu ya hisia, yenye kunyanyasa kusikoelezeka. Sikuwa nimefikiria kwanza kuwa hayakuwa haki au yalikuwa si sahihi.

Nikasikia sauti yangu, si sauti ya mtu au sauti ya Mungu, ilikuwa ni sauti yangu, lakini sikuiongea. Labda ilikuwa dhamiri yangu, mimi sijui, lakini ni dhahiri niliisikia ikisema, "*Omba kwa Mungu !*" Kwa hiyo, nilijiwazia mwenyewe, "*Siamini katika Mungu.*" nilikuwa nafikiri, "*hata kama ningepomba, mimi sijui jinsi ya kuomba kabisa.*"

Wakati huo, mimi sikuwa nimeomba kwa miaka 23. Nilipokuwa mtoto, tulisema maombi katika shule ya jumapili (Sunday school) na Kanisani. Nilijaribu kuyakumbuka. Kwangu mimi, kuomba ilikuwa kama mtu anayekumbushia kitu alichokisoma.

" *Bwana ni mchungaji wangu, Tupe leo mkate wetu wa kila siku, nchi yangu tis' ya hivi. subiri, haya si maombi. Naam nijapopita katika njia ya bonde la uvuli wa mauti, kwa alama na miaka saba iliyopita baba zetu ...* " Nilianza kujichanganya tu, sikuweza kukumbuka jinsi ya kuomba.

Kila mara nilipotaja neno Mungu kwa watu hawa walionidhuru, ilikuwa ni kama nawarushia maji ya moto juu yao. walilia, kupiga mayowe na kelele. Walitumia lugha chafu mbaya sikuwahi kusikia katika dunia hii. hawakuweza kuvumilia kuwa karibu yangu napozungumza juu ya Mungu. Ilikuwa inawauma sana kwa uchungu wanaposikia kuhusu Mungu kiasi kwamba walikaa mbali nami. Basi, nilianza kuwa na hisia kwamba ninaweza kuwazuia kwa kuongea habari za Mungu. Kwa hivyo nilijaribu kukumbuka sala, lakini nilikuwa najichanganya mwenyewe.

Hatimaye nilitambua kwamba wameondoka na niko peke yangu. Mimi nalikuwa huko peke yangu milele, Ninachomaanisha sikuwa najua muda wowote. Lakini nilifikiri kuhusu maisha yangu, na kuhusu yale niliyo yafanya, niliwaza kwa ile hali niliyokuwa nayo. hitimisho nililokuwa nalo ni kwamba maisha yangu yote ya utu uzima nimekuwa na ubinafsi, na mungu wangu ilikuwa ni mimi mwenyewe. Niligundua kwamba kulikuwa na tatizo kwenye maisha yangu, na kwamba watu waliokuwa wanamishambulia walikuwa ni watu

wenye maisha kama yangu hapa duniani. Hawakuwa mizimu,wala mapepo; walikuwa ni watu waliokosa IT. Walipokuwa hai hapa duniani, walikuwa wamekosa hivi vitu, waliishi maisha ya ubinafsi na ukatili. Na sasa mimi nilikuwa katika dunia ambayo kulikuwa na hakuna kitu kingine, zaidi ya ubinafsi na ukatili. Walikuwa wamewekwa kuumizana wenyewe kwa wenyewe, milele. Na sasa mimi nilikuwa ni sehemu yao.

Ingawa mimi sikutaka kuwako pale, lakini niliona kama mahali pale ni haki niwepo. Nilihisi kuwa pale pana nistaili, kwa sababu hivi ndivyo nilivyoishi. Huwezi kupata picha jinsi nilivyokuwa nasikia uchungu wa hisia. Nimelala pale kwa wakati usio na mwisho, nikifikiri juu ya hatma yangu.

Nyuma ya fikira zangu ikaja picha yangu mwenyewe nilipokuwa mtoto nilikuwa nimekaa kanisani katika shule ya jumapili (Sunday school) darasani, nikiimba Yesu ananipenda. “Yesu ananipenda,la la la,Yesu ananipenda.” Nilijisikia mimi mwenyewe nilipokuwa mtoto nikiimba. Cha kushangaza zaidi ni kuwa niliweza kuhisi hivyo moyoni mwangu.

Kulikuwa na wakati katika maisha yangu nilipokuwa kijana na sikuwa na hatia na niliamini katika kitu kizuri, niliamini kwa habari ya mtu mwingine zaidi ya mimi mwenyewe, niliamini kwa huyo ambaye alikuwa na vitu vyote vizuri, mwenye nguvu zote, ambaye alikuwa ananijali sana na nilitaka kile ambacho nilikipoteza, nilikitupa, nilisaliti, nilikihitaji tena. lakini sikuwa namjua Yesu, lakini nilihitaji kumjua Yesu. Sikufahamu upendo wake, lakini nilihitaji kujua upendo wake. Sikuwa najua kama kweli alikuwa ni halisi, nilihitaji awe halisi. Kulikuwa na wakati katika maisha yangu ambapo niliamini katika kitu hicho fulani,na na nilitaka kuamini kwamba kweli ile ilikuwa ni kweli.

Hivyo nikaita nikiwa gizani, “*Yesu, tafadhali niokoe!*” Mara ya kwanza kulikuwa na vipande vidogo vya mwanga kule gizani, kwa haraka vikakua na kuangaza sana. Mwanga ukawa mkubwa sana kiasi kwamba katika ulimwengu wa mwili ungeweza kunila. Ungeweza kunibanika kama kipande cha chipsi.Lakini haukuwa na moto au na hatari pale. Alikuwa ndani ya mwanga huu alifika chini na taratibu akaanza kuninyanyua.

Kwenye mwanga huu niliweza kuona kuwa niko kwenye utukufu, bado mchafu na vidonda kila sehemu. Nilifanan kama aliyegogwa na gari pembeni mwaa barabara. Kwa taratibu akaweka mikono yake chini yangu na akaninyanyua kwa upole. Alipokuwa akinigusa, vidonda vyote, maumivu na uchafu vikaondoka. Vikatoweka, kabisa na nikaponywa kabisa nikiwa mzima. na ndani, nikiwa nikiwa nimejazwa upendo wake. Natamani ningeelezea. Inanichanganya kuona kwamba siwezi kuwaelezea jinsi nilivyokuwa nikijisikia kwa sababu ilikuwa ni kitu kizuri ambacho hakijawahi kunitokea katika maisha yangu, ilikuwa ni kila kitu kwangu. Ilikuwa ni Maisha yote kuufahamu Upendo wake, na siwezi kuwafunulia hiki kitu.

Kwa hiyo akanikumbatia, akanibembeleza, akanifuta mgongo wangu, kama mtoto akimfanyia mwanae, kama mama akimfanyia binti yake, kwa upole alinifuta mgongo wangu. Nilikuwa kama mtoto ndani ya furaha; nilipotea sasa nimepatikana, nilikufa sasa nimerudishwa kwenye uhai. Akawa ananibeba nje na pale, na tukaondoka nje.Tulikuwa tukielekea kwenye ulimwengu wa Mwanga,na nikaanza kujisikia aibu kubwa. Nilikuwa mtu mbaya sana, nilijifikiria mwenyewe kuwa mimi ni mchafu , nanuka,takataka. Nikafikiria mwenyewe, “*Amfanya makosa, sistahili kuwepo hapa, Anihitaji mahali hapa*” Anawezaje kunijali na sasa tunapaa.

Kisha tukasimama tulikuwa hatupo kuzimu wala mbinguni, tulikuwepo katikati. Akasema, “ *Hatufanyi makosa , wewe unapaswa kuwepo hapa,*” tukaanza mazungumzo na akaanza kunieleza vitu.



Aliniletea malaika ambao walikuwa pamoja nami tokea mwanzo mpaka mwisho. Walinielekeza kilicho sahihi na kisicho sahihi. Na ilikuwa ni rahisi tu. Nilipokuwa mtu wa upendo , nikiwajali wengine, iliwafanya malaika wafurahi, ilimfanya yesu afurahie, na waliniacha nijue kwamba ilimfurahisha Mungu pia. Na nilipokuwa mbinafsi na mnyonyaji

iliwafanya malaika wasifurahi, na Yesu alikuwa hana furaha wakati huu na kwamba hata Mungu hakuwa na furaha. Walichokuwa wanajaribu kusema nami kwa ufupi ni kuwa kusudi langu la kuishi ilikuwa ni kumpenda Mungu na kuwapenda jirani zangu kama ninayojipenda. Hii ndio maana naliumbwa, hiyo ndiyo iliyonifanya niwe hapa duniani na kujifunza. Lakini nilishindwa.

Waliniambia kuwa nilitakiwa kurudi kwenye dunia hii, na nikashangaa kabisa kwa sababu nilitaka kwenda Mbinguni. Walichoniambia ni kuwa mbinguni ilikuwa ni sehemu ambayo ni ya furaha, kufurahisha na sehemu ya ajabu sana. Kila mtu angependa kwenda Mbinguni na nilitaka kuwepo pale. Waliniambia kuwa sikuwa tayari, Sikuwa nimestahili, ilikuwa si wakati wangu kwenda mbinguni bado. Ilikuwa ni wakati wangu wa kurejea tena hapa duniani na kujitahidi kuishi katika njia impendezayo Mungu, jinsi alivyoniumba niishi.



Nilimwambia Yesu na malaika kwamba sitaweza kuishi katika dunia hii bila wao. Niliwaambia kwamba moyo wangu ungevunjika kama ningerudi tena katika dunia hii. Watakuwa pale na mimi nitakuwa hapa. Wakaniambia Tumekuwa na wewe muda wote huu. Na wewe hujawahi kuwa peke yako pale chini. Wao wakaniambia, *"Huelewi? Tatizo ni nini? Tunakuonyesha haya yote. Tumekuwepo pale siku zote. Tumekuwa nawe siku zote pale. Na haujawahi kuwa peke yako pale."*

Mimi nikasema, *"Mnatakiwa mniambie kwamba mtakuwa karibu yangu mara moja kwa muda tu."* Basi wakaniambia kama mimi nikiomba na kukiri dhambi yangu kwa Mungu, kama nikitoa kile nilichonacho kwa Mungu, yaani nimkabidhi wasiwasi wangu, vitu navyojali sana, matumaini, na ndoto zangu, yote mkabidhi Mungu, basi kutakuwa na wakati nitajua katika moyo wangu kwamba wako pamoja nami. Si lazima kuwaona, lakini nitahisi upendo kama niliohisi wakati huo. Niliwaambia kuwa kama wao watanihaki kishia kuwa kuna wakati mimi naweza kuhisi upendo huo, basi naweza kuishi katika dunia hii. Walisema watafanya hivyo, kisha wakanirudisha tena.

Baada ya tukio hilo, nesi ambaye alisema kuwa hawakuweza kupata daktari, akrudi mbio kwenye chumba na kusema kuwa daktari amefika. Katika hospitali hii ni muujiza kwa sababu hii ilikuwa kama saa 3 au 3:30 usiku. Alisema " daktari amefika katika hospitali na tunakwenda kukufanyia upasuaji moja kwa moja." Na baadhi ya ... watu wakaja na wao wakamtoa mke wangu nje ya chumba. Ilinisumbua sana kwa sababu nilikuwa najaribu kuwaambia nilitaka kumwambia mke wangu yaliyotokea kwangu. Hivyo wakati nampita mke wangu kuelekea kwenye upasuaji, nalisema kila kitu kinaenda kuwa safi. Na yeye akaanza (?) kujiuliza..., huyo ni kama mtu anayekufa. Jambo la ajabu kuhusu uzoefu huu ni kuwa kumbukumbu haikupotea wakati wote. Ni kweli ilikuwa kazi na sifahamu jinsi ilivyokuwa kazi. Naamini moja ya sababu ya kuwa Mungu alinipa mimi uzoefu huu ni kwamba nipate kuwa na nafasi ya kushiriki kwa mtu mwingine ushuhuda huu. Mimi sijui nani na kamwe sijui ni nani. Lakini napenda kuchukua fursa hii kushiriki na mtu ili iwe msaada kwao.

=== *Street Interviews* ===

**(Yohana 14:6)**

*<sup>6</sup>Yesu akamjibu, "Mimi ni njia, na ukweli na uhai. Hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu.*

**[Announcer]**

Uchunguzi uliofanyika umebaini kuwa watu wengi hawaamini katika Mbingu ya kweli na kuzimu. Na wengi wao wanaoamini kuwa sehemu hii ipo, wanamitazamo tofauti, jinsi mtu anakwenda kutoka hatua moja kwenda nyingine.



**[Random Person on Street #1 (Man)]**

*Siamini kwa habari ya Kuzimu. Nina amini kuna Mbingu. Ndiyo kuna uwezekano kabisa kwamba kunazaidi ya maisha haya tunayoishi hivi sasa ambayo ni muda mfupi kwenye Dunia, Kunakitu kinachofuatia baada yake.*



**[Random Person on Street #2 (Man)]**

*Naamini kila mtu atalipa kile wanachofanya katika maisha. Siamini kwa ulazima kile Biblia inasema kuhusu Kuzimu kuwa sehemu kuungua kwa moto, Naamini kuzimu ni hofu za mtu zanzomsumbua sana na kila kitu ambacho ni uovu kwa mtazamo wako mwenyewe, Utalipa kwa umilele wote. NA Mbingu ni mahali ambapo unaishi maisha yako kwa amani kama tu unampenda Mungu na unaishi kama Mungu na unaishi kwa neno lake. I*



**[Random Person on Street #3 (Woman)]**

*Naamini kuna Mbingu, kweli kuna Mbingu. Sina uhakika sana kwa habari ya Kuzimu. Unaelezeaje Kuzimu. ingawa, Mbinguni Ndiyo.*



**[Random Person on Street #4 (Man)]**

*Sifikirii kwamba kuna ulazima wa kwenda kanisani ili kwenda Mbinguni, au kwamba unaamini katika Biblia, Lakini ishi maisha mazuri. Kuzimu iko kwa ajili ya wachache ambao ni wabaya, kwa mfano mtu fulani atakayeya kwa kukusudia. Nadhani Uuaji ndiyo dhambi pekee itampeleka mtu Kuzimu.*



**[Random Person on Street #5 (Woman)]**

*Sina uhakika kitu gani kitakupeleka Kuzimu, au kwa nini uende Mbinguni. Siwezi kujua.*



**[Random Person on Street #6 (Man)]**

*Nadhani hakuna Mbingu au Kuzimu kwa uhalisia, mara baada ya maisha haya. Sifahamu kwa uhakika ni nini hasa. Sifahamu hasa pale kuna nini, lakini ninafikiri kuna ukatikati, au unusu, au purgatory ambapo kila mtu anakwenda. Si pazuri sana au pabaya sana.*



**[Random Person on Street #7 (Woman)]**


*Ninaamini kila mtu katika fikira zao wanafikiri kwa habari ya Mbingu na Kuzimu. Mbingu ni kile kinachowapa furaha, kile wanachokitazama mbele, na kile wanachokiamini “kwa imani zao wenyewe”, iwe ni Mungu au miungu au kitu, kwamba Mbingu ipo. Na hicho ndicho wanachofanyia kazi katika maisha. Binti yangu yeye ni atheist ( haamini katika Mungu), lakini nyuma ya fikira zao, anajua kuna kitu ambacho angependa nje ya maisha haya. Na hicho kwangu mimi ndiyo kinachohitajika, muungu hauhitajiki.*



**[Random Person on Street #8 (Woman)]**

*Ninaamini katika imani yangu mwenyewe ambayo ni zaidi ya imani hii ya ulimwengu huu (metaphysical). Ninaamini jinsi unavyojisikia duniani, unavyotazama mbingu, kwamba ni kitu gani, ni mtazamo wako mwenyewe. Na ndivyo inavyokuwa ukifa. Hivyo kama unaamini kwamba kuna muungu ambaye yuko ndani yako, na kwamba wewe ni mtu mzuri, na mtu mwenye furaha, hicho ndicho kinachotokea kama ukifa. Lakini siamini kuwa unaadhibiwa, na unaenda mahali palipojaa moto, kwa sababu haukuishi jinsi dini mbalimbali zinavyosema uishi.*

**[End of Interviews]**



**[Dr. Rawlings]**

Watu weni wanajaribu kuchakachua ujumbe huu wa kuzimu na mbinguni wakisema kwamba hakuna sehemu kati ya hizi ni halisi. Kwa nini hatuli, hatunwi na hatuoi? Kama hakuna kuwajibika, basi hakuna dhambi. Na kama hakuna dhambi, Kristo alikufa bure. Na kama Kristo alikufa bure, Tunamuhitaji Mungu ili iweje? Hii ni filsofia mpya ya Zama hizi mpya, kwamba hakuna Kuzimu. Ni matumaini ya wengi kwamba hakuna kuzimu.

Washiriki wanakwenda kwenye mahospitali, kutembelea wapendwa wetu na ujumbe wa Zama mpya. Unaitwa dini ya miaka ya mwisho, dini ya uzoefu wa watu waliokaribia kufa wakisema, “*Angalia, nilikwenda mbinguni*”, wanamwambia mgonjwa anayekaribia kufa, “*Niliona mwanga na nikaja*”. *Kila kitu ni safi. Hakuna kuwajibika, hakuna kuzimu. Mageti ya Mbinguni yako wazi kwa kila mmoja anayekufa. niangalie. Niangalie mimi ni atheist na niko hapa. Hautakiwi kuhofu. Kifo si kitu cha kuhofia. Nitakwenda kukaa pamoja nawe. Familia yako inaogopa kukaa na wewe unapokuwa ukifa, lakini siogopi. Ngoja nikamate mkono wako, Ngoja nikueleze kuhusu kitu hiki chenye utukufu kinachokuja kukuchukua, huu mwanga mzuri mwishoni mwa njia ambapo hakuna hofu, hakuna hasara, ni faida tu. Unapokelewa kama ulivyo. Hakuna mbingu, hakuna kuzimu. Ni milele kwa wote.*” Hii ndio filsofia ya zama mpya wanaojiita Omega Faith, kwamba kila mtu anakwenda mbinguni. Kuna vikundi vya watu hawa wanaokuja kwenye hospitali zetu, wanakutana na watu wanaokufa, badala ya vikundi vyetu vya makanisa yetu kuja na kukutana na hawa wanaokufa.

Huduma kwa wanaokufa ni huduma ambayo imeachwa sana. Hakuna anayeipenda. Kila mtu anaogopa mgonjwa anayekufa. Na mgonjwa anayekufa anataka kujua kufa kuna maana gani. Je inaumiza? Je kuna maisha baada ya kufa? Je kuna Mbinguni na Kuzimu? Ninawezaje kuwa na uhakika kwamba nitakwenda mbinguni? Na wewe unaweza ukwaambia kwamba ni zawadi ya bure. Unaweza kuwaeleza jinsi ya kupata kitun hiki. Lakini kama hatutajitetea sisi wenyewe na imani hii ya Omega, ambao wanapenyeza kwenye hospitali zetu na imani ambayo ni hatari kama kufa, basi tutakwenda kupoteza ukristo wetu. Mgonjwa atakufa uchi bila imani yoyote ile.

**=== Dr. Donald Whitaker ===**



Kesi yetu nyingina inayofuata ni ya Dr. Whitaker ambaye bado anafanya majukumu yake, lakini alikuwa ni atheist wakati wa tukio. Alikuwa afanyi chochote kinachohu siana na Mungu, lakini kunahali ambayo ilibadili maisha. Tungependa ushiriki hicho pamoja na ye.



**[Dr. Donald Whitaker]**

Ilikuwa ni mwezi wa pili 1975, wakati nilipokuwa mlevi wa pombe kupindukia. Pia nilikuwa nikitumia madawa ya kunipa raha. Lakini kimsingi, pombe ilikuwa ni dawa yangu ya pekee. Nilikuwa niko mlevi sana. Nilikuwa na marafiki wengi kwenye biashara ya burudani; Ringo star na kikundi kingine cha watu.

Walikuwa na kipindi maalumu cha TV pande za west coast. Haight (*rafiki*) aliniita na kuniuliza kama ningeweza kwenda. Nilimweleza kuwa nitapenda kwenda, kwa sababu nilijua kutakuwa na pombe na mambo ya burudani mengi sana. Walipokuwa wakifanya mambo yao mimi nilifanya yangu. Baada ya muda wa siku



tatu au nne, nikawa mgonjwa. Nilipatwa na maumivu makali ya tumbo. Nilipanda ndege mpaka jiji la Oklahoma, nikamuita rafiki yangu seneta, na nikamueleza anitumie gari kwa ajili yangu kwa kuwa nilikuwa mgonjwa. Wakaniletea gari ikanichukua mpaka nyumbani. Na nikaangalia katika Hospitali ya Whatley pale Texarkana, Texas februari 1975. Nikafanya uchunguzi wa afya yangu kwa electrolytes, hii inamaana kuwa kemikali kwenye mwili wangu hazikuwa kwenye mlingano, kiasi kwamba iliwabidi wanipe IVs ili kunjenga tena.



Wakati wote huo wa maisha yangu nilikuwa ni atheist. Nilikuwa atheist ali yekubuhu na nilikuwa nikii shi mimi kama mimi tu. Atheist ni wabinafsi, wana shi kwa wanavyojisikia. Hivi ndivyo nilijikuta mwenyewe hospitali mwaka 1975.



Baada ya siku 3 walinifanyia upasuaji. Baadae, nilijikuta mwenyewe kwenye chumba cha watu mahututi ikiwa kwenye mashine za kupumulia, ambayo ilikuwa ndiyo hewa yangu. Sikuweza kuongea. Nilikuwa pale katika komma. Niliwasikia hawa watu wakiongea jinsi nilivyokuwa mgonjwa na jinsi nitakavyo kwenda kufa na jinsi nitakavyo toka nje ya hospitali. Wakati ule nywele zangu zilikuwa ndefu sana kwa sababu nilivaa urefu wa nywele zangu. Na nikamsikia jamaa mmoja akisema “nywele zangu ni ndefu”, na mwingine akasema, “Si mbali na kutokea wakati huu atakwenda kuondoka mahali hapa.” Na sauti ya tatu ikasema, “hawezi kuondoka mahali hapa. Atakwenda kufa,”

Na baada ya siku ya 3, niliweza kupumua mwenyewe. Niliweza kumkumbuka dakitari wangu, mpasuaji wangu, Dr. Donald Dunkon akisema nami, “Don, kama unachochote cha kuweka sawa, kama unakitu chochote cha kusaini, ni vyema ukafanya sasa kwa sababu hatuna uhakika ni muda gani wa kuishi ulionao.”

Nafahamu nilikuwa na tatizo linaloitwa Acute hemorrhagic narcotic pancreatitis. Huwezi kuishi na ugonjwa huu. unaweza kuishi na pancreatitis. unaweza kuishi na acute pancreatitis, lakini huwezi kuishi na Acute hemorrhagic narcotic pancreatitis. Dunkon aliwaeleza watoto wangu wawili kwamba nitakufa kabla ya asubuhi. Hawakutaraji mimi kuishi.



Nilikuwa nimelala pale, nikijitambua kama atheist. Sikuamini katika Mungu. Niliamini katika nguvu ya Dunia/anga kwa sababu nimeiona. Mimi kama muuguzi nimehusika na kifo na maisha. Niliamini katika kitu fulani lakini usiniambie habari za Mungu. Na kwa hakika situtaka mtu aniambie kwa habari ya ufufuo, bikira kuchukua mimba au aina yeyote ya vitu kama hivyo kwa sababu niko katika uchunguzi (research) na sayansi. Wengi wao wenye PHDs za research na sayansi hawaamini katika Mungu. Hawaamini katika nguvu iliyojuu ya nguvu zingine zote. Wanaanza kuamini kwamba kuna mpangilio tu wa anga ya dunia kwa sababu zaidi huko tunapokwenda tunaona huu mpangilio.

Ni rahisi kuwa atheist unapokuwa umefanikiwa. Umetembea katika nji yako mwenyewe kutoka katika hali ya maisha ya Oklahoma na kuwa mmoja kati ya watu wenye nguvu katika sana katika jimbo la Oklahoma, kisiasa. Ni rahisi sana kuwa atheist unapokuwa umefanya hayo yote. Mtu anaweza akakaa na kusema “Simuhitaji Mungu. Mungu ni Nani?”

Ni vigumu sana kuwa atheist, unapokuwa umelala kwenye kitanda ukisubiri kufa, kwa sababu unaanza kuwaza “ itakuaje kama hawa wakristo wako sahihi?” Kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa anaitwa Ron

Short, ambaye alisimama katikati yangu na milango ya kuzimu. Mtu mmoja alinishuhudia kuhusu upendo wa Yesu kwa miaka 5, kabla sijawa mgonjwa, kwa sababu alisema atafanya kile kitu ambacho atakwenda kufanya. alikuwa ni mmoja kati ya wale waliosema kuwa ni wakristo na wanaishi yale waliyoyasema watayafanya. Nilimuheshimu sana. Sikuwa naamini alichokisema lakini nilimuheshimu.

Nilipokuwa nimelala na nikifahamu kuwa nitakwenda kufa, fikiri ni nani nilimfikiria? Nilifikiri, “*Vipi kama Ron yuko sahihi? Vipi kama kuna Mbingu na Kuzimu*” Kwa haraka wazo lililokuwa na nguvu kwenye fikra zangu ni jinsi gani ninaokoka. Kuokoka ni nini?Ninaokokaje?

Hivyo nikatuma watu waende kumchukua Ron Short. Nilitaka aje kwa sababu nilitaka afanye vile anaweza kufanya. Sikuwa na wazo mtu aliyening’inia kwenye mti kule Israeli miaka 2000 iliyopita anaweza kunisaidia. hiyo ni nini kwangu? Lakini nilifahamu alikuwa na kitu ambacho nilitakiwa kuwa nacho. Usiku huo Ron hakuwa nyumbani, alikuwa Alabama. Nikawaeleza watu waende na kumchukua Ron.

Usiku ule ulikuwa ni usiku mrefu ambao sikuwahi kuwa nao katika maisha yangu, kabla au tangu. Nilipokuwa nimelala pale kitandani, nikaanza kupoelea kwenye giza. Ilikuwa ni giza. Ilikuwa kama giza linapenya ndani kabisa kwenye mwili wako. Nitakueleza tu kwamba niliuacha mwili wangu kwa sababu ninakumbuka nilipokuwa narudi tena kwenye mwili wangu. Sikuwa nafahamu nilikuwa wapi nje ya mwili wangu.

Kuna watu wanaongelea kuhusu mwanga, au kuelea juu, hisia ya upendo na wema. Lakini sikuhisi chochote kati ya hivyo, sikuhisia hata kimojawapo cha hayo, Nilihisi hofu kuu isiyoelezeka. nilijua kwamab kama nikiendelea mbele, sitaweza kurudi tena. Ndani yangu kabisa nilijua hivyo. kwa hiyo nilipigana usiku mzima.



Walinieleza baadae kuwa si tu kwamba nilivuta shuka ya godoro nje ya godoro, niliweka godoro juu yangu, nilitakiwa kukaa, ilinibidi nisubiri mpaka Ron aje pale. Chochote atakachofanya, ilinibidi nimsubiri.

Lakini tena nilipokuwa nikiuacha mwili wangu, nilikuwa nakwenda chini kwenye giza nene la kutisha. Ngozi yangu ilianza kuwa na baridi. Sio baridi unayoisikia unapokuwa nje ya hewa, hapana, hii ilikuwa ni baridi inayochoma kwenye mifupa. Na nilikuwa nahisi ubaridi ukija kwenye miguu yangu.

Tena nilikuwa nikiondoka kwenye mwili wangu na nilikuwa kwenye giza, kwenye ule uwazi kama shimo. Nakumbuka wakati fulani nilikuwa nikiingia kwenye mwili wangu, Nilihisi mwili wangu ulikuwa unapiga, mwili wangu wan je unajipigiza. Niamini, niamini, huo ulikuwa ni wakati wa kuogopesha na ambao sikuwahi kukutana nao.

Nilipigana usiku mzima. Asubuhi iliyofuata. Kwenye mida ya saa 3:30 au saa 4 kamili, Ron akaingia ndani. Akasema, “*Dr. Whitaker, wanasemaje kuhusu nafasi ya kuishi?*” “*Nikasema, “Ron wananiambia sina Muda wa kuishi.” akasema “Sasa ni muda” Nikasema “Uko sahihi.”*”

Kabla, nilishawahi kumlaani, nilishawahi kumtemea mate, lakini sasa ulikuwa ni wakati kwa sababu nilitakiwa kuwa nacho chochote alichonacho. Nilikuwa nina muda mchache umebakia kwenye dunia na sikuwa na wazo ni lini nitafaya hiyo safari na kuondoka.



Wakati huo Ron aliniongoza kwenye maombi ya mwenye dhambi. Sikuwa najua nini maombi ya mwenye dhambi yalikuwaje, Lakini nilimuamini Ron. Aliniongoza kwenye maombi ya mwenye dhambi

na akaniambia Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako. Alikufa kwa dhambi za ulimwengu. sikuelewa mapema kuhusu hilo. akanionyesha katika neon la Mungu imeandikwa wapi.

Unatakiwa uelewe hili kwamba mimi ni mtu wa vitabu. Nimetumia muda wangu mwingi sana, miaka 25 au 26 kwenye vitabu, vitabu vya sayansi vya aina zote. Nina digrii za chemia, safari yote hiyo mpaka kuwa dakitari wa kemia ya vitendo.

Aliniambia na nikamuamini kwa sababu imeandikwa kwenye kitabu, kilichoitwa Biblia. Nikamuona Ron akinisomea, na nikasema sala ya toba. Nitakueleza kitu kimoja, kulikuwa na amani ilikuja na kunivaa vile sijawahi kujua.

Nimetafuta amani kwenye chupa, pombe, sindano, madawa na wanawake. Nimeitafuta katika sehemu zote hizo. Lakini hakukuwa na amani katika maisha yangu. Lakini nilipompokea Yesu kuwa bwana na mwokozi wa maisha yangu, sikuogopa tena. Niliendelea kuamini kuwa bado ningekufa kwa sababu ya hali yangu ile niliyokuwa nayo, na huwezi ukapona. Nilifahamu hivyo, mimi ni tabibu. Nilijua kile nilichonacho huwezi kupona.



Ron alinionyesha kwenye neon la Mungu paliposema, “showed me in the word of God where it says, *“Ishara hizi zitaambatana na waaminio. Wataweka mikono kwa wagonjwa nao watapata afya”* (Marko 16:18) Nilitembea katika sayari hii siku hii, sikuchukua insulin, sikuchukua enzymes, nilikula nilichohitaji, na kila siku Mungu anatengeneza katika mwili wangu vitu vya mimi kufanya bila kuchukua tiba yeyote.



Unapooona macho yasiyoona yanaona, unapooona walemavu wanatembea, unapooona wako ma wanatakasika, na unawaona kwa macho yako kabisa, kwa hivyo haichukui sayansi ya rocket kufikiri kwamba Biblia ni kweli.

[Dr. Rawlings]

Ni namna gani hatua tofauti za kuzimu zinasura tofauti kwa watu? Biblia haisemi kuwa ni moto kila eneo. Ukiangalia sehemu tofauti tofauti, inasema;

- “Kutupwa nje”
- “Kutengwa mbali na Mungu”
- “Giza kuu”
- “Kwa minyoo isiyokufa”

Sehemu kubwa ni moto. Kuona malaika wa nuru wakati mwingine inaweza kuwa ni uongo. Kwa mfano, [2 Wakorintho 11:14](#), inatambia kuwa hata Shetani anaweza akajibadilli mwenyewe kuwa malaika wa nuru na kuwadanganya wengi. Ni mwanga upi ambao watu hawa waliuona mwisho wa tanuru, hasha kama ilikuwa ni fulani ambaye hakuwaza kuwepo peponi? Manbo hayo hutokea.

Cha kushangaza zaidi kinyume chake huwa hakitokei. Wale wote wanaojikuta Kuzimu wanafahamu kabisa wapi imewapasa kuwa. Na hawajiulizi ni kwa nini wamewekwa pale. Ukweli, hata Yesu aliongelea hili katika Mathayo 25. Yesu akasema pia shetani akimtoa shetani mwenzie ufalme wake utafananaje? (mathayo 12:26) Ina maana, kwa nini shetani hawaonyeshe watu ushuhuda wa kuzimu, ambao utafanya kazi kinyume na ufalme wake na uongo wake. Haiwezekani. Kama malaika wa Nuru, shetani anadanganya watu au labda ni moto. Lakini utofauti huu wanaouona kuzimu, iwe ni giza kuu au moto, sehemu zote hizo ni sehemu ambazo wasingependa kurudia tena.

Hii inatupeleka kwenye kesi ya Dr. George Rodonaia, Kijana wa kirussia, mwenye akili. alikuja na Ph.D na M.D, lakini alikuwa na shida na KGB. Hakuweza kutoka nje ya Russia. na kwa uhakika ni kwamba kila alipokuwa akijaribu kutoka nje ya Russia, alipelekwa chini kwa makusudi na ajenti wa KGB, aliyemgonga pembeni mwa barabara na akampitia kwa juu. Na hivi ndivyo alivyokufa na hadithi yake ilipoanzia..

[Dr. George Rodonaia]

Kama psychiatrist and a neuropathologist, kwangu mimi Mungu hayupo. sikuwahi kuamini katika mungu. sikuamini katika biblia. sikuwaza kwa habari ya Mungu, sikuwaza kwa habari ya Mungu, biblia au dini. Mwaka 1976, Nilipokuwa na miaka 20 nilikuwa tayari ni dakitari nikifanya kazi Georgia, Russia.

Nilikutana na msichana kutokea Texas. nilijaribu kuondoka inchini mara kadhaa. Lakini sikuwa na msaada wa kutosha. Huyu msichana alijitahidi kunisaidia na nikaingia kwenye matatizo makubwa na KGB. Nilifanya kazi na “idenotriphosper”, ilikuwa ni kisafirishaji cha neuroni kwenye ubongo. Kunapotokea muingiliano wa "Oxitocin", Ninagundua vitu vingi.

Nilikuwa ni mwanasayansi mashuhuri na KGB hakutaka mimi niondoke hivyo wakaamua kuniua. hapo ndipo nilipokutana na mwonekano mwingine wa maisha.

Nilisimama kando ya barabara, tayari kabisa kwenda NY, nilikuwa nikisubiri usafiri wa tax, ndipo nilipogongwa na gari pale pembeni mwa barabara. Niliruka hewani mita 10, na gari ikanitembelea juu yangu. Ndugu na rafiki zangu wakanipeleka hospitali. Wauguzi wa hospitali, marafiki zangu na maprofesa 2 wakasema nimekufa. Ijumaa usiku, wakaniweka kwenye friji za maiti mochwari.



Siku tatu baadae, wakanitoa nje.Sasa jumatatu asubuhi wakaanza kunifanyia autopsy.Hizi siku 3 za kutokuwepo kwenye mwili wangu, nikiangalia kila kitu ambacho kilinitokea,

nilikuwa nikijiona, mwili wangu, niliona kuzaliwa kwangu, wazazi wangu, mke wangu,mtoto wangu na marafiki zangu. Ni liweza kuona mawazo yao. Niliweza kuona kile wanachowaza. Jinsi mawazo yao yalivyokuwa yanatembea kutoka mwonekano mmoja na mwingine.


Ilikuwa ni uzoefu wa kushangaza. Nilikuwa katika giza, giza kuu. Giza lilinigandamiza, giza hili liko si nje lakini kutokea ndani. ninachoweza kusema giza lilinigandamiza. Na nilikuwa

katikati ya hofu hii na sikuelewa kwa nini na namna gani giza hili linakuwepo. Nilikuwa wapi?

Nilifahamu kwamba sikuwa na mwili kwa sababu sikuhuhisi. lakini nikaona mwanga. Nilienda kwenye shimo dogo. lakini mwanga ulikuwa mkali sana, unaoangaza sana. Huwezi ukaufananisha na mwanga wowote ule. Hakuna maneno yanayoweza kuelezea. Mwanga huu uliwaka, ukapita mpaka ndani ya mwili. lakini sikuwa na mwili wa nyama. Hiyo ndiyo ilikuwa sehemu ya kushangaza.

Nilikuwa nikiogopa sana ule mwanga, nilitamani kwenda kwenye kivuli kujiziba mwenyewe kutoka kwenye mwanga huu. Huo ulikuwa ni mwanga upi? Sijui. Inaweza ukaitwa ni mwanga wa Mungu,inaweza ikaitwa mwanga wa maisha. Lakini mwanga ni mwanga na giza ni giza. Mimi kama Psychiatrist na mwanasayansi, sikufikiria hicho, Kitu kizuri ni kuwa nilikuwa katika mwanga.

Hatukuwa tumekulia katika njia ya Mungu. Unafahamu jumuiya ya kisoviet(urusi), hatukuwa tunaenda kanisani. Kulikuwa kuna watu wanaoenda.Lakini walikuwa ni wachache sana. Nafikiri awakufahamu zaidi kama sisi tulivyodhania kuwa hakukuwa na mungu. Lakini hizo siku 3 za kuwepo mochwali, kwenye friji, zilibadili maisha yangu.



Wakaanza kunifanyia autopsy,na walipoanza kukata kifua change. hiyo ilikuwa ni mara yangu ya kwanza, nikafungua macho mara,na nikaona wanafunzi wangu wakiogopa, wakaanza kunywea. Walipoona macho yangu yanachezacheza kwenye mwanga wakajua kuwa nilikuwa ni mzima.wakanirudisha tena hospitali na kuanza matibabu ya kunirejesha (resuscitation).

Mapafu yangu yalishindwa kufanya kazi kwa muda mrefu hivyo niliwekwa kwenye mashine za kupumulia kwa siku 90. Kuponaa kwangu hakukutokea kwa haraka, lakini maisha yalikuja tena. Waligundua ya kwamba maiisha yalikuwepo wakati wanafanya autopsy, lakini sio viungo vyangu vyote vilikuwa vinafanya kazi. Ilikuwa ni kazi ya muda wa miezi tisa nikiwa bado naendelea kupona, haikutokea kwa haraka,lakini maisha yalikuwepo pale. Lakini madaktari walinisaidia mimi kupona na wakanisaidia kuanzisha afya na viungo vyangu tena.

Nilipokuja kwenye maisha tena, nilipatwa na mambo mengi sana. Niliweza kukataliwa, nilikorofishana na wengine wengi. Lakini hakuna kungebadilisha fikra zangu, Nilifahamu mwisho wangu, njia yangu.Niliamua kuondoka nchini , na huyu dada kutokea longview Texas alinisaidia kuhamia United States(USA). Tulienda texas na kuamua kuishi mpaka hivi leo.

Wakati mwingine mambo yapo juu ya uwezo wetu wa kufikiri. Lakini sitajaribu kuelezea yote kwa sababu nafahamu na kuamini kwamba Mungu anafahamu zaidi. Naamini kwamba sihitaji kuelezea kila kitu. Lakini kwa nini ilionyeshwa kwangu mimi na kwa nini nilichaguliwa mimi? Ni swali ambalo siku zote nimekuwa silitilii maanani. Najali kwamba ninaamini kwa undani Mungu wa upendo na Mungu ni upendo. Naamini Mungu aliumba kia kitu kwa ajili ya uzuri na kwa ajili ya makusudio/hatima njema kama tu hatutayaharibu.

---

**=== CPR Instructions ===**

*Full instructions at <http://globalcrisis.info/cpr.html>*



**[Dr. Rawlings]**

Na sasa nataka nikuonyeshe kwa habar ya CPR. Tulisema tungekuonyesha jinsi ya kuanzisha moyo wa mtu tena na kuanzisha upumuaji wao tena. unafanya hivyo kwa mikono yako iliyowazi . kwanza anaangalia kama mtu yuko sawa. Labda yeye amedhurika. Je, yeye yuko tayari kuzungumza na wewe ? Labda amejibamiza kichwa chake. unaangalia kwa haraka, unahisi na kusikiliza kama anapumua mara moja kifua kinafanya miemuko, pua inahema? Je hewa yeyote unahisi? Kama hapana hewa unayohisi, nenda

kwenye njia ya hewa, achana na moyo, utahusika na moyo baada ya njia ya hewa.

Hauzui njia ya hewa kwa kunyanyua kidevu, na kukielekeza juu ya paa. Hii inanyoosha njia ya hewa. Kisha unafunga pua zake ili kwamba hewa itapumulia mapafu. Unampa pumzi mbili za haraka. Na unaangalia kama diaframu yake inapanda. Kama inapanda basi, haijazuiliwa. Lakini kama bado imezuiliwa unakwenda tena kumpa pumzi 2 na unasogela mpaka kwenye mdomo wake kwenye sehemu inayozuiliwa. Kama moyo wake hauptumui, unakagua kwa kutokusikiliza na pua lakini kwa kuhisi kwenye upande wa tunda la Adamu , bom,bom,bom.



Kama hausikii hicho, baada ya pumzi mbili za kumpumulia, nchi 2 juu ya xiphoid, upande wowote wa mfupa wa kifua, diaframu, chini ya mfupa wa kifua, unaweka kiganja cha mkono, kikifuatiwa na kingine kwa juu. Sukuma uzito kwa chini yake.

Hii ni wakati ambao wa muhimu sana, kama unaweza kuwapata watu kabla ya kufa na kuwapa uamuzi huu wa kumkubali Yesu Kristo kama mwokozi wao, basi hawawezi kupoteza hata kama wanaishi au kufa. Hii iko pamoja nao siku zote. Na kama wakifa kama hivi hatuna sababu ya kujiuliza wamekwenda wapi. Na muhubiri atakuwa sawa kama akisema wamekwenda mbinguni kuwa na Mungu.

Lakini kwa wale wanaokufa barabarani, wanakwenda wapi? Ni changamoto kwa wahubiri, kwako wewe na mimi kwa nini hatukuwaendea kwa injili ambayo ni karama ya bure kwa yeyote anayeitaka.

---

**=== Conclusion ===**

Huu uzoefu wa kuzimu wote unakitu ambacho kinafanana. Kinashangaza! Hawakuwa wanafahamu kama kuna hiyo sehemu. Je ,nawe utashangaa? Je nitashangaa? Au tutakuwa tumejiandaa? Kuzimu si ktu kipya.Imekuwepo pale siku zote. Watu hawa wamevumbua kuwa kama tukifa na kurudi. wanataka kukuambia kuhusu yenyewe.

**[Dr. Rodonaia]**

Na nimejua nini maana ya Upendo, Imani ni nini,Tumaini ni nini.Na mambo yote haya 3 ni Hekima ya Mungu.

**[Dr. Whitaker]**

Maombi ya imani, maombi ya wokovu, sio maombi fulani madogo,ndio njia pekee ya kwenda kwa Baba.Na ndio njia pekee. Sasa wale watu wote wa harakati ya Zama Mpya wanaoamini kila mtu atakwenda mbinguni, kwamba unaweza kuabudu chochote, unaweza kuabudu nzi, unaweza kusogeza mti,unaweza kuabudu jiwe,unaweza kuabudu nyota.Nina habari kwa niaba yao, hawataenda isipokuwa wamempoke Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao, kwa sababu neon linasema njia pekee ya kwenda kwa baba ni kupitia Mwana.

**[Ronald Reagan]**

Usiende kuzimu,Tafadhali,nakuomba.Usiende kuzimu. Haikuindaliwa kwa ajili yako.

**[Charles McKay]**

Kama umeokoka, umeokoka, kama tu ukimpokea Yesu

**[Howard Storm]**

Usiweke hiki kitu ukafanya iwe kesho, kwa sababu yeyote ile, kwa sababu unaweza ukafa wakati huu sasa.

**[Charles McKay]**

Ni kitu kizuri ambacho kimewahi kutokea katika maisha yangu.

**[Howard Storm]**

Unaweza kuhisi uwepo wa Yesu uko pamoja nawe,leo, mahali hapa wakati huu.

**[Ronald Reagan]**

Sio mpango wa Mungu kwamba watu waangamie.Sikuwa nafahamu hili. Sikuwa nafahamu upendo wa Mungu. Nilichofahamu ni chuki,vurugu,na unyanyasaji.Lakini kuna mmoja anayejali. Jina lake ni Yesu.

**[Whitaker]**

Na mwana ni nani? Yeye ni neno alifanyika mwili na akaja na akakaa pamoja na wanadamu. Neno ni njia ya kwenda kwa Baba.

**[Howard Storm]**

Fanya uamuzi. Sio kesho, sio usiku, Fanya uamuzi sasa. Je unakwenda kutoa moyo wako kwa Yesu au hapana?

**[Charles McKay]**

Kama unataka kuwa na maisha baada ya haya ni vyema umkubali Yesu.

**(Ufunuo 3:20)**

*<sup>20</sup>Sikiliza! Mimi nasimama mlangoni na kubisha hodi. Mtu akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia nyumbani kwake na kula chakula pamoja naye, naye atakula pamoja nami.*

[Dr. Rawlings]

Rafiki, umesikia ushahidi. Hii iko karibu na unavyokwenda kufanya maamuzi. Je kuna maisha baada ya kifo? Je watu hawa uliowasikia waliyabadili maisha yao juu chini bure tu ,au kwa sababu kuna mbingu na kuzimu?

Umekwisha fanya uamuzi huu katika maisha yako? Unauhakika kuwa kama ukifa leo hii utakuwa na Mungu mbinguni? Kumbuka mstari kutoka Ufunuo 3:20,Tazama nasimama mlangoni nabisha .Mungu anabisha hivi sasa. Kama ukinisikia, fungua mlango nami niingie. Nitaingia, si kwamba ninaweza kuja , na kufanya ushirika pamoja nawe , nawe pamoja nami. Hii inamaana unakuja ukiwa mchafu, jinsi ulivyo. Atafanya ushirika pamoja nawe na kukueleza jinsi ya kusafisha maisha yako.Na baada ya hayo,anakupa karama ya bure ya uzima wa milele na Yesu Kristo kwa sababu wewe unakuwa kitu kimoja pamoja naye. Sasa unakuwa Mkristo.

(Yohana 11:25-26)

<sup>25</sup>Yesu akamwambia, "Mimi ndimi ufufuo na uhai. Anayeniamini mimi hata kama anakufa, ataishi; <sup>26</sup>na kila anayeishi na kuniamini, hatakufa kamwe. Je, waamini hayo?"

**The End**  
**To Hell and Back**  
by Dr. Rawlings Documentary

*Ndugu aliyefasiri ufunuo huu ni Peter Kahale ni kijana aliyeokoka na anampenda Yesu na mwenye shauku ya kuhubiri injili ya Yesu Kristo.*

*Simu ya Mkononi: +255-755-255043, +255-653-610460.*

*Barua Pepe: kahalepeter@gmail.com.*